



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE



Tarehe: 16/05/2023

## YAH: TANGAZO LA AJIRA YA MUDA YA MSIMAMIZI WA MIRADI

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe anakaribisha maombi kwa kila mradi kutoka kwa watanzania wenye sifa kwa ajili ya kusimamia miradi ifuatayo:-

- i) Ujenzi wa shule mpya ya msingi Kiwira.
- ii) Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika shule ya msingi Goye.
- iii) Ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na choo cha matundu manne katika shule ya msingi Katumba II.
- iv) Ujenzi wa madarasa mawili na matundu matatu ya vyoo katika shule za msingi za Ibililo, Ikuti, Bulyaga na Masebe.
- v) Ujenzi wa vyumba vitatu na matundu matatu ya choo katika shule ya msingi Mwankenja.

### Majukumu ya Msimamizi wa Mradi

- i) Kutoa ushauri na maelekezo ya kitaalamu kwa vibarua wanaotekeleza mradi.
- ii) Kuainisha mahitaji ya mradi husika wakati wa utekelezaji.
- iii) Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa shughuli za kila siku za mradi.
- iv) Kusimamia utekelezaji wa mpango kazi, kuandaa na kutoa taarifa ya utekelezaji wa mradi kwa timu ya usimamizi kila siku.
- v) Kufanya tathmini ya maendeleo ya mradi na kutoa taarifa kwa timu ya usimamizi.
- vi) Kuratibu upatikanaji wa vibarua na mikataba yao.

### Sifa za Mwombaji:

- i) Awe na elimu ya kidato cha IV na au cha VI.
- ii) Awe na shahada/stashahada ya juu ya Uhandisi (Civil Engineer) au Mkadiriaji Majenzi (Quantity Surveyor) au Mchoraji (Architecture) kutoka vyuo vikuu vinavyotambuliwa na serikali.
- iii) Mwombaji awe na umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- iv) Mwombaji awe hajawahi kutenda kosa la jinai.

2. Maombi yatumwe kwa:-

Mkurugenzi Mtendaji,

Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe,

S.L.P. 148,

**TUKUYU.**

**NB:** Tangazo hili linapatikana pia kwenye Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ambayo ni [www.rungwedgec.go.tz](http://www.rungwedgec.go.tz).

Limetolewa na:



Mchau, R. B

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA**

**RUNGWE. MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
RUNGWE**

3. Maombi yanapokelewa kuanzia tarehe 16/05/2023 hadi tarehe 23/05/2023 saa 9:30

Alasiri.